# AckySHINE.com

# Maana ya jina Bikira Maria

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · February 17, 2020

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Bikira Maria

Jina asili kwa Kiaramu ni ????, Maryam lenye maana ya "Bibi"; watafsiri wa kwanza wa Biblia ya Kiebrania wanaojulikana kama Septuaginta (LXX) waliliacha kama lilivyo wakiandika kwa Kigiriki ?????u, Mariam, au walilifupisha wakiandika ?????, Maria.

Katika Kurani jina hilo kwa Kiarabu ni ????, Maryam.

Jina hili limeenea sana duniani kote, hasa kwa heshima ya mama wa Yesu.

Anatajwa kwa kawaida kwa kutanguliza sifa yake mojawapo, hasa Bikira.

Mapokeo ya karne ya 2 (Injili ya Yakobo) kuhusu Bikira Maria yanasema alikuwa binti pekee wa Yohakimu na Ana. Lakini habari muhimu zaidi ni zile zinazopatikana katika Biblia ya Kikristo.